JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA MLIMBA

**MUHTASARI WA KIKAO CHA KAWAIDA ROBO YA TATU (JANUARI – MACHI) CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA TAREHE 01/02/2022 KATIKA OFISI YA MWENYEKITI WA HALMASHAURI(W)**

**MAHUDHURIO**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Witness R.Kimoleta | Mwenyekiti |
| 2. | Suleiman Maseko | Katibu |
| 3. | Colex A. Mwakyelu | Mjumbe |
| 4. | Dr Christina L. Guveti | Mjumbe |
| 5. | Elias M. Malinjanga | Mjumbe |
| 6. | Wakili,Nakua F.A | Mjumbe |

**WASIOHUDHURIA**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Joseph E. Mgana | Kwa taarifa |

**SEKRETARIETI**

1. EUNICE Y. MHILU

**MUHTASARI NA. TB/16/02/2022 – KUFUNGUA KIKAO**

Katibu alimkaribisha mwenyekiti,Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe kwa kuwasihi kupitia taarifa zilizowasilishwa kwa makini ili kutoa maamuzi sahihi na kufungua kikao mnamo saa 8:30 mchana .

**MUHTASARI NA. TB/17/02/2022 – KURIDHIA AJENDA**

Ajenda tisa(9) ziliwasilishwa.Wajumbe walipokea na kuridhia agenda hizo ziwe mwongozo wa kikao.

Ajenda hizo ni;

1. Kufungua kikao
2. Kuridhia Ajenda

3. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha bodi ya zabuni cha tarehe 30/11/2021

4. Kuthibitisha manunuzi yaliyofanyika kwa njia ya mzunguko (circular resolution)
5. Kutunuku kazi zifuatazo baada ya kupitia mapendekezo ya timu ya tathimini.
    a) Fundi ujenzi wa nyumba ya Mtumishi Hospital ya Wilaya.
    b) Fundi wa kutengeneza na kufunga madirisha ya vioo majengo ya Utawala,Kufulia,Bohari ya dawa na Mionzi.
    c) Fundi wa kutengeneza madawati 450 ya wanafunzi shule za msingi.
    d) Fundi wa kujenga kichomea taka na shimo la kutupa kondo la nyuma.
6. Kuidhinisha manunuzi ya Vifaa na huduma kwa Idara na Vitengo mbalimbali.
7. Kurithia Ongezeko la gharama za fundi ujenzi wa miundombinu ya maji taka jengo la OPD na Maabara.
8. Mengineyo
9. Kufunga kikao

**MUHTASARI NA. TB18/02/2022 – KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI CHA TAREHE 30/02/2021.**

- Wajumbe wa bodi ya zabuni walipitia muhtasari wa kikao cha 30/02/2021 na kuuridhia baada ya marekebisho machache yakiuandishi kufanyika;-

**MUHTASARI NA. TB/19/02/2022 – KUTHIBITISHA MANUNUZI YALIYOFANYIKA KWA NJIA YA MZUNGUKO**

- Wajumbe walipitia manunuzi yaliyofanyika kwa njia ya mzunguko (circular resolution) na.11 na walilidhia kuwa kumbukumbu ya Halmashauri.

**MUHTASARI NA. TB/20/02/2022 –KUTUNUKU KAZI ZIFUATAZO BAADA YA KUPITIA MAPENDEKEZO YA YA TIMU YA TATHIMINI.**

a) **Fundi ujenzi wa nyumba ya mtumishi Hospital ya Wilaya.**
Baada ya Wajumbe wa bodi ya zabuni kupitia mapendekezo ya timu ya tathimini na PMU walikubaliana na mapendekezo hayo kwa kumpitisha fundi Vitusi Mwambike aitwe kwenye timu ya majadiliano ili aweze kujenga nyumba hiyo kwa kiasi cha Tsh. 13,500,000.00 sawa na 15% ya Tsh. 90,000,000.00 ambayo ndiyo fedha ya mradi iliyopokelewa kwa muda miezi 3.

b) **Fundi wa kutengeneza na kufunga madirisha ya vioo majengo ya Utawala,Kufulia,Bohari ya dawa na Mionzi.**
Wajumbe wa baada ya kupitia mapendekezo ya timu ya tathimini walikubaliana kazi hii ya kutengeneza madirisha ya vioo kwa majengo ya Utawala,Kufulia,Bohari ya dawa na Mionzi ifanywe na Leo Aluminum and Glass kwa kiasi cha Tsh.43,239,800.00 kwa muda wa siku 28.

c) **Fundi wa kutengeneza madawati 450 ya wanafunzi shule za msingi.**
Baada ya wajumbe wa bodi ya zabuni kupitia mapendekezo timu ya tathimini yaliyowasilishwa walikubaliana kazi hii ya kutengeneza madawati 450 kazi hii ifanywe

na ujenzi wa shimo la kutupa kondo la nyuma apewe fundi Reuben Walker Mteri kwa kiasi cha Tsh. **1,536,000.00/=** kwa muda wa siku 28.

**MUHTASARI NA. TB/21/02/2022 – KUIDHINISHA MANUNUZI YA VIFAA NA HUDUMA KWA IDARA NA VITENGO MBALIMBALI.**

**a. UJENZI WA JENGO LA HALMASHAURI.**

- Ununuzi wa vifaa vya bomba (mfumo wa maji) hatua ya ujenzi wa Jamvi vyenye Jumla ya Tsh.**6,295,500.00/=** Mzabuni JAKEMS INVESTMENT LTD.
- Ununuzi wa vifaa vya umeme kwa ajili ya kuunganisha umeme wa muda kutoka jengo la OPD hadi eneo la Ujenzi wa Ofisi za Halmashauri kwa jumla ya Tsh: **1,400,000.00/=** Mzabuni SHIJA HUSEIN MDEE

**b. UJENZI WA MAJENGO MATANO HOSPITAL YA WILAYA**

- Ununuzi wa mbao kwa ajili ya kumalizia hatua ya blundering jengo la Utawala na mama na mtoto Kwa Jumla ya Tsh. **2,240,000.00/=** Mzabuni SHIJA MDEE.
- Ununuzi wa Saruji mifuko 400 kwa ajili ya umaliziaji wa majengo manne (mionzi,kufulia,utawala, mama na mtoto) ya Hospital ya Wilaya,kwa kiasi cha Tsh:**6,600,000.00/=** Mzabuni VUNJABEI INVESTMENTS CO
- Ununuzi wa vifaa vya mfumo wa maji ujenzi wa jengo la Utawala Hospital ya Wilaya kiasi cha Tsh: **3,435,500.00/=** Mzabuni JAKEMS INVESTMENT LIMITED.
- Ununuzi wa vifaa vya umeme na maji kwa ajili ya kukamilisha mfumo wa maji na umeme jengo la mama na mtoto Hospital ya Wilaya kwa kiasi cha Tsh: **7,057,000.00/=** Mzabuni SHIJA HUSEIN MDEE.

**MUHTASARI NA. TB/22/2/2022– MENGINEYO**

- Wajumbe walikumbushia umuhimu wa wao kupata mafunzo kwa ajili ya ufahamu Zaidi juu ya utekelezaji wa majukumu yao kwa ufanisi

**MUHTASARI NA. TB/23/2/2022 – KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa Kufunga kikao saa 10:00 jioni

UMETHIBITISHWA

.......................................... KATIBU

.......................................... MWENYEKITI

09/03/2022
..............................
TAREHE